

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA WAZIRI MKUU

### KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

#### TAARIFA KWA UMMA

#### **WITO KWA WAAJIRI KUSHIRIKI KUTOA MAFUNZO YA VITENDO MAHALI PA KAZI KWA WAHITIMU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA JULAI 2017 / JUNI, 2018**

- Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu** inapenda kuutaarifu umma wa Watanzania hususan Waajiri na Makampuni kuwa, kwa kushirikiana na Wadau inatekeleza Programu ya Taifa ya miaka mitano ya Kukuza Ujuzi wa Nguvu Kazi ya Taifa (2015/16 – 2020/21). Lengo kuu la programu hii ni kuwezesha nguvu kazi ya taifa hususan vijana kupata ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa kwenye sekta mbalimbali katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi. Mafunzo ya vitendo kwa wahitimu mahali pa kazi (internship training) ni moja ya vipengele muhimu vya programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi. Mafunzo ya vitendo kwa wahitimu mahali pa kazi yamekusudiwa kuwezesha vijana wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kupata uzoefu wa kazi kwa kuoanisha ujuzi walioupata darasani na mahitaji ya soko la ajira na hivyo kuongeza uwezo wa kuajirika katika soko la ajira.
- Ofisi ya Waziri Mkuu, inawakaribisha Waajiri na makampuni yote katika sekta mbalimbali za kiuchumi na ngazi zote kushirikiana na Serikali kutoa mafunzo ya ujuzi kwa wahitimu kwa kutoa fursa kwa wahitimu kujifunza katika maeneo yao ya kazi katika kipindi cha Julai 2017 hadi Juni 2018. Tunapenda kuwataarifu waajiri kuwa, kwa kuwa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu mahali pa kazi si ajira, waajiri hawatalazimika kuingia gharama za ziada kwa kutoa fursa kwa vijana kufanya mafunzo ya vitendo katika maeneo yao ya kazi. Ofisi ya Waziri Mkuu itagharamia masuala gharama za msingi kuwezesha vijana husika kumudu gharama muhimu katika kushiriki mafunzo husika.
- Hivyo, tunapenda kuwaalika Waajiri wote kushiriki mpango huu kwa kujiandikisha na kujaza fomu maalum inayopatikana kupitia tovuti ya Ofisi: [www.kazi.go.tz](http://www.kazi.go.tz). Maombi yawasilishwe kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu, Mwalimu Nyerere Pension Tower, 42 Barabara ya Bibi Titi**

**Mohamed, P.O. BOX 1422, 11480 Dar es Salaam kufikia tarehe 30 julai 2017 au kwa barua pepe: ps@kazi.go.tz.**

4. Tunapenda kuujulisha Umma na Waajiri kuwa mpango huu utahusisha vijana wahitimu wa elimu ya juu katika fani na taaluma zote isipokuwa kwa zile taaluma ambazo mafunzo ya vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu hufanyika kama sehemu ya mandeleo ya kitaaluma kwa mujibu wa sheria husika.

**IMETOLEWA NA:  
KATIBU MKUU**